

JIFUNZE KICHINA



每日汉语

斯瓦希里语 02



国家汉办/孔子学院总部
Hanban/Confucius Institute Headquarters



中国国际广播电台
CHINA RADIO INTERNATIONAL

中国国际广播出版社

02

JIFUNZE KICHINA

每日汉语

中国国际广播出版社



目录 / Yaliyomo

第十五课 吃小吃

Somo la 15 Kula chakula cha aina mbalimbali 1

第十六课 家庭聚会

Somo la 16 Kula chakula katika familia
ya wachina 8

第十七课 宴会

Somo la 17 Tafrija 15

第十八课 在超市

Somo la 18 Katika Supamaketi 21

第十九课 水果市场

Somo la 19 Soko la matunda 27

第二十课 二手市场

Somo la 20 Soko la bidhaa zisizo mpya 32

第二十一课 电话购物

Somo la 21 Kuagiza bidhaa kupitia simu 37



目录 / Yaliyomo

第二十二课 在服装店

Somo la 22 Kwenye duka la nguo 43

第二十三课 在商场

Somo la 23 Kwenye duka 50

第二十四课 在书店

Somo la 24 Kwenye duka la vitabu 57

第十五课 吃小吃

Somo la 15 Kula chakula cha aina mbalimbali



A: Kwanza tunarudia maneno tuliyojifunza kwenye somo la 14:

Qīng nǐ men děng yí huì er.

1. 请 你 们 等 一 会 儿。Tafadhali subirini kidogo.

Wǒ men yào děng duō jiǔ?

2. 我 们 要 等 多 久? Tunatakiwa kusubiri kwa muda gani?

Wèi dao zěn me yàng?

3. 味 道 怎 么 样? Unaonaje ladha ya chakula?

Zhēn de hěn hǎo chī.

4. 真 的 很 好 吃。Ladha ni nzuri kweli.

Wǒ chī bǎo le.

5. 我 吃 饱 了。Nimeshiba.

A: Sasa tuanze somo la 15:



今日关键 Maneno mapya ya leo

Nǐ men xǐ huan chī là de ma?

1. 你 们 喜 欢 吃 辣 的 吗? Mnapenda kula chakula cha pilipili?

Wǒ xǐ huan chī yáng ròu chuàn.

2. 我 喜 欢 吃 羊 肉 串。Napenda kula mshikaki wa nyama ya kondoo.

Zhè lǐ miàn shì shén me?

3. 这里面是什么? Ndani ya chakula hiki ni nini?

Wǒ men qù mǎi diǎn yǐn liào ba.

4. 我们去买点饮料吧。Twende tukanunue vinywaji.

A: Katika mikoa ya Sichuan, Hunan na sehemu nyingine nchini China, watu wanapenda kula chakula chenye pilipili, na siku hizi wasichana wengi pia wanapenda kula chakula chenye pilipili, ukienda kwenye mkahawa pamoja na marafiki zako, kwanza unaweza kuwauliza, 你们喜欢吃辣的吗? Mnapenda kula chakula cha pilipili?

B: 你们喜欢吃辣的吗? Matamshi yake kwa herufi za kiswahili ni: **ni men xi huan chi la de ma**

A: 你们 **ni men**, ninyi, 喜欢 **xi huan**, penda, 吃 **chi**, kula, 辣的 **la de**, chakula cha pilipili, 吗 **ma**, kisaidizi cha neno.

B: 你们喜欢吃辣的吗? **ni men xi huan chi la de ma**

对话一 Maongezi ya kawaida ya wachina (1)

A: 你们喜欢吃辣的吗? Mnapenda kula chakula cha pilipili?

B: 你们喜欢吃辣的吗? **ni men xi huan chi la de ma**

A: 喜欢。Tunapenda.

B: 喜欢。xi huan

A: Lakini mimi napenda kula mshikaki wa nyama ya kondoo. 我喜欢吃羊肉串。

B: 我喜欢吃羊肉串。wo xi huan chi yang rou chuan

A: 我 wo, mimi, 喜欢 xi huan, penda, 吃 chi, kula, 羊肉串 yang rou chuan, mshikaki wa nyama za kondoo.

B: 我喜欢吃羊肉串。wo xi huan chi yang rou chuan

对话二 Maongezi ya kawaida ya wachina (2)

A: 你想吃什么? Unataka kula nini?

B: 你想吃什么? ni xiang chi shen me

A: 我喜欢吃羊肉串。Napenda kula mshikaki wa nyama ya kondoo.

B: 我喜欢吃羊肉串。wo xi huan chi yang rou chuan

A: Mshikaki wa nyama ya kondoo hakika unapikwa kwa nyama ya kondoo, lakini kama unataka kujua chakula fulani cha kichina kama *Jiaozi*, ambacho umbo lake ni kama sambusa, ndani kuna nini, unaweza kuuliza, 这里

面是什么? Ndani ya chakula hiki ni nini?

B: Oh, ni rahisi sana, 这里面是什么? **zhe li mian shi shen me**

A: 这里面 **zhe li mian**, ndani ya kitu hiki, 是 **shi**, ni, 什么 **shen me**, nini.

B: 这里面是什么? **zhe li mian shi shen me**

对话三 Maongezi ya kawaida ya wachina(3)

A: 这里面是什么? Ndani ya chakula hiki ni nini?

B: 这里面是什么? **zhe li mian shi shen me**

A: 我也不知道。Mimi pia sijui.

B: 我也不知道。 **wo ye bu zhi dao**

A: Lakini kama ukiona kiu kweli, unaweza kumwambia rafiki yako mchina: 我们去买点饮料吧。Twende tukanunue vinywaji.

B: 我们去买点饮料吧。 **wo men qu mai dian yin liao ba**

A: 我们 **wo men**, sisi, 去 **qu**, kwenda, 买 **mai**, nunua, 点 **dian**, chache, 饮料 **yin liao**, vinywaji, 吧 **ba**, kisaidizi cha neno.

B: 我们去买点饮料吧。 **wo men qu mai dian yin liao ba**

对话四 Maongezi ya kawaida ya wachina(4)

A: 我们去买点饮料吧。 Twende tukanunue vinywaji.

B: 我们去买点饮料吧。 **wo men qu mai dian yin liao ba**

A: 你喜欢红茶还是绿茶? Unapenda chai nyekundu au chai ya kijani?

B: 你喜欢红茶还是绿茶? **ni xi huan hong cha hai shi lu cha**

A: 你 **ni**, wewe, 喜欢 **xi huan**, penda, 红茶 **hong cha**, chai nyekundu, 还是 **hai shi**, au, 绿茶 **lu cha**, chai ya kijani.



Vidokezo vya utamaduni

Kuhusu vijiti vya kulia vya kichina na vijiko, baadhi ya watu wanaona kuwa, China ni nchi ya kilimo, vyakula vikuu vya China ni nafaka na mboga, hivyo watu wanatumia vijiti kula chakula. Na nchi za magharibi nyingi zilikuwa ni nchi za kufuga mifugo, vyakula vikuu vyao ni vya nyama, hivyo wanapendelea kutumia vijiko. Mbali na hayo, wachina wa familia moja hula vyakula pamoja, ambapo vitoweo huwekwa kwenye sahani moja

moja kwenye meza moja, hivyo watu wanatumia vijiti vya kulia kuchukua kitoweo kila mara. Na kwa wazungu, kila mtu ale vyakula vyake kwenye sahani yake. Jambo linalosisitizwa ni kuwa, ni mwiko kwa wachina kupachika vijiti vya kulia kwenye wali au kupiga bakuli kwa vijiti vya kulia.



第十六课 家庭聚会

Somo la 16 Kula chakula katika familia ya wachina



A: Kwanza tunarudia maneno tuliyojifunza kwenye somo la 15:

Nǐ men xǐ huan chī là de ma?

1. 你们喜欢吃辣的吗? Mnapenda kula chakula cha pilipili?

Wǒ xǐ huan chī yáng ròu chuàn.

2. 我喜欢吃羊肉串。Mimi napenda kula mshikaki wa nyama ya kondoo.

Zhè lǐ miàn shì shén me?

3. 这里面是什么? Ndani ya chakula hiki ni nini?

Wǒ men qù mǎi diǎn yǐn liào ba.

4. 我们去买点饮料吧。Twende tukanunue vinywaji.

A: Sasa tuanze somo la 16:



今日关键 Maneno mapya ya leo

Wǒ hěn gāo xìng rèn shi nǐ de jiā rén.

1. 我很高兴认识你的家人。Nafurahi kufahamiana na watu wa familia yako.

Zhè shì wǒ de ná shǒu cài.

2. 这是我的拿手菜。Hiki ni kitoweo nilichopika vizuri.

Ni duō chī diǎn er.

3. 你多吃点儿。Ule zaidi.

Xià cì qǐng nǐ men dào wǒ jiā zuò kè.

4. 下次请你们到我家作客。Siku zijazo mnakaribishwa nyumbani kwangu.

A: Ukienda nyumbani kwa rafiki yako wa kichina, unaweza kusema: 我很高兴认识你的家人。Nafurahi kufahamiana na watu wa familia yako.

B: 我很高兴认识你的家人。Matamshi yake kwa herufi za kiswahili ni: **wo hen gao xing ren shi ni de jia ren**

A: 我 **wo**, mimi, 很 **hen**, sana, 高兴 **gao xing**, kufurahi, 认识 **ren shi**, kufahamiana, 你的 **ni de**, yako, 家人 **jia ren**, watu wa familia moja:

B: 我很高兴认识你的家人。

对话一 Maongezi ya kawaida ya wachina (1)

A: 欢迎你来作客。Karibuni nyumbani.

B: 欢迎你来作客。 **huan ying ni lai zuo ke**

A: 欢迎 **huan ying**, karibu 你 **ni**, wewe, 来 **lai**, kuja, 作客 **zuo ke**, kuwa mgeni.

A: 我很高兴认识你的家人。Nafurahi kufahamiana na

watu wa familia yako.

B: 我很高兴认识你的家人。wo hen gao xing ren shi ni de jia ren

A: Wakati ukiwa mgeni wa nyumbani kwa wachina, wachina hupenda kukupikia chakula kitamu, na wanataka wewe uonje na kukwambia: 这是我的拿手菜。Hiki ni kitoweo nilichopika vizuri.

B: 这是我的拿手菜。zhe shi wo de na shou cai

A: 这 zhe, hiki, 是 shi, ni, 我的 wo de, changu, 拿手 na shou, kufanya vizuri, 菜 cai, kitoweo.

B: 这是我的拿手菜。

对话二 Maongezi ya kawaida ya wachina (2)

A: 这是我的拿手菜, 你尝尝。Hiki ni kitoweo nilichopika vizuri, tafadhali uonje.

B: 这是我的拿手菜, 你尝尝。zhe shi wo de na shou cai, ni chang chang

A: 不错。挺好吃的。Tamu sana.

B: 不错。挺好吃的。bu cuo. ting hao chi de

A: Wakati wa kula chakula nyumbani kwa wachina, wachina huweza kukutaka ule chakula kingi zaidi, husema: 你多吃点儿. Ule zaidi.

B: 你多吃点儿. **ni duo chi dian er**

A: 你 **ni**, wewe, 多 **duo**, nyingi, zaidi 吃 **chi**, kula 点儿 **dian er**, kisaidizi cha neno.

B: 你多吃点儿. **ni duo chi dian er**

对话三 Maongezi ya kawaida ya wachina(3)

A: 你多吃点儿. Ule zaidi.

B: 你多吃点儿. **ni duo chi dian er**

A: 我吃饱了. Nimeshiba: 我 **wo**, mimi, 吃 **chi**, kula, 饱 **bao**, shiba, 了 **le**, kisaidizi cha neno.

B: 我吃饱了. **wo chi bao le**

A: 下次请你们到我家作客. Siku zijazo mnakaribishwa nyumbani kwangu.

B: 下次请你们到我家作客. **xia ci qing ni men dao wo jia zuo ke**

A: 下次 **xia ci**, siku zijazo, 请 **qing**, tafadhali, 你们 **ni men**, ninyi, 到 **dao**, fika, 我家 **wo jia**, nyumbani

kwangu, 作客 **zuo ke**, kuwa wagoni.

B: 下次请你们到我家作客。 **xia ci qing ni men dao wo jia zuo ke**

对话四 Maongezi ya kawaida ya wachina(4)

A: 下次请你们到我家作客。 Siku zijazo karibuni tena nyumbani kwangu.

B: 下次请你们到我家作客。 **xia ci qing ni men dao wo jia zuo ke**



Vidokezo vya utamaduni

Tarehe mosi mwezi wa kwanza kwa kalenda ya kichina ni sikukuu ya Spring ya China, yaani sikukuu ya mwaka mpya wa China. Sikukuu hiyo ni sikukuu kubwa kabisa ya China. Kwa kufuata mila na desturi za kichina, watu husafisha na kupamba nyumba ili kutarajia kusherehekea sikukuu ya mwaka mpya. Kwa mfano, watu hupenda kubandika “春联” (**chūn lián**), karatasi mbili nyekundu zinazoandikwa maneno ya matumaini ya mwaka mpya. Mbali na hayo, baadhi ya watu wanatundika taa kubwa nyekundu, na kubandika maandishi ya kichina ya kutakia heri na baraka “福” (**fú**) na picha ya Budha